


Huduma za Kikristo za Tony Alamo
Jarida la Dunia
Yerusalemu Mpya
Makanisa Ulimwenguni Kote
Mchungaji Tony Alamo | Taifa la Kikristo la Alamo | Toleo 20100

# MAJARIBIO MATATU YASIYOFANIKIWA KUMPINDUA MUNGU

**na Tony Alamo**

Je, haikuudhi kwamba Shetani ameidanganya dunia nzima? Amefanya haya katika matukio matatu ambapo, wazi wazi amejaribu kuchukua nafasi ya MUNGU na Ufalme wa MUNGU. Majaribio yake mawili yameshindwa vibaya, na hili la tatu analofanya sasa hivi litashindwa hivi karibuni.

Jaribio la kwanza la Shetani kumpindua MUNGU lilikuwa katika bustani ya Edeni, wakati Shetani alipomuuliza Hawa, "Hivi ndivyo alivyosema MUNGU?" Mwanzo 3: 1-3 inasema, "Basi nyoka [Shetani] alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya BWANA MUNGU. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema MUNGU, Msile matunda ya miti yote ya bustani? Mwanamke [badala ya kukemea na kumkataa] akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula." Lakini MUNGU alisema, kuhusu matunda ya mti wa katikati ya bustani, "Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa." Wakati MUNGU anasema "msije mkafa," YEYE hasemi kifo ni cha muda mfupi, jambo la dakika. Humaanisha kifo ni mauti ya milele kwa roho ya mwanamme au mwanamke, milele katika moto wa Jehannamu, mauti ya milele. Ukweli wa jambo hili umeelezwa katika Maandiko ya Agano la Kale na Jipya.[1]



*Wachungaji Tony and Susan Alamo na bendi kwenye kipindi chao cha kimataifa cha televisheni* *picha ilipigwa mwaka 1974*

Mwanamke, kama ilivyo kwa wakazi wengi wa dunia, kamwe hawaoti kwamba unapokubali hoja za Shetani, unakubali umilele unaoogofya na kutisha, Jehannamu isiyokuwa na mwisho, ambayo ina athari zaidi zinazochizisha kwa pamoja roho na akili ya muhanga wake. Kuzimu itacheua moshi wa maumivu ya waovu milele (Ufunuo 14:9-11). Wale wanaomwabudu (yaani kumsikiliza) Shetani, serikali yake ya dunia-moja, na kanisa lake la dunia (Katoliki) watakumbwa na mauti hayo hayo.[2] Shetani katika umbo la nyoka, hufanya hila, kama alivyomdanganya Hawa, na sasa anadanganya dunia nzima.[3]

Katika kitabu cha Ufunuo 12:9, Shetani ameelezewa kama joka kubwa. "Yule joka akatupwa, yule mkubwa [kutoka Mbinguni], nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote." Shetani alijua kwamba kwa kumdanganya Hawa, angeweza kuihukumu dunia nzima.[4] Hawa alikuwa mwinjilisti wa kwanza wa Shetani; alikuwa mbuzi wa kwanza. Ili kuwa mbuzi wa Shetani, huwezi kumwamini YESU, au kuwa mmoja wa wanafunzi WAKE. Huwezi kuishi maisha ya KRISTO ya kusulubiwa, bali utalazimika kuwa huru kutenda yanayokupendeza. Huwezi kumshuhudia KRISTO bali kumkana, YEYE AJAYE ulimwenguni kuwaokoa wadhambi.[5]

Wakati Shetani alipomwambia Hawa kwamba, hakika hamtakufa, mtakuwa kama MUNGU, hivyo basi kula na umpe Mumeo naye ale, Hawa akafanya kama alivyosema (shetani), na akamuhubiria mumewe. Mara wakafumbuliwa macho (Mwanzo 3:7). Walitambua kuwa wamekuwa wadhambi, na kwamba walikuwa wamedanganywa. Utawala wa dunia sasa ni mali ya Shetani badala yao, na hakuna kitu tena ila kuwa na imani katika kifo cha baadaye cha KRISTO na ufufuo vinaweza kuwarejesha kwa MUNGU.

Awali, MUNGU aliwabariki Adamu na Hawa kuliko viumbe wote. Akawapa mamlaka juu ya ulimwengu wote, kila ki-

*(Inaendelea ukurasa wa 2)*

**1** Zab. 9:17, Isa. 5:11-15, 33:10-14, 66:24, Mat. 3:12, 5:29, 7:13, 8:11-12, 10:28, 13:38-42, 47-50, 18:6-9, 22:8-13, 25:31, 41-46, Mk. 9:42-48, Lk. 3:17, 16:19-26, 2 The. 1:7-9, 2 Pet. 2:1-9, Yud. 5-7, Ufu. 14:9-11, 19:20, 20:15, 21:8, 27 **2** Ufu. 13:1-8, 14:8-11, 17:1-15, 18:1-8 **3** Mwa. 3:1-6, Isa. 14:9-17, Mat. 24:11-12, 24, 2 Kor. 4:3-4, 11:13-15, 2 The. 2:3-12, 2 Tim. 3:13, Ufu. 13:1-8, 11-18, 16:13-14, 17:1-2, 8, 18:2-3, 23 17:8, 19:19-21, 20:1-3, 7-10 **4** Rum. 5:12-21, 1 Kor. 15:20-22 **5** Mat. 20:28, 26:28, Yn. 1:29, 3:14-17, 6:51, 10:11-18, 11:49-52, Mdo. 5:30-31, 20:28, 26:23, Rum. 5:6-11, 1 Kor. 15:3-4, Gal. 1:3-4, 2:20, 4:4-5, Efe. 5:2, 1 Thes. 1:10, 5:9-10, 1 Tim. 2:5-6, Tit. 2:13-14, Ebr. 2:9-10

## MAJARIBIO MATATU YASIYOFANIKIWA KUMPINDUA MUNGU

*(Inaendelea kutoka ukurasa wa 1)*

umbe hai. Mwanzo 1:28 inatuambia kuwa MUNGU akawaambia, "Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha: Na mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi." Adam na Hawa walikuwa watawala wa dunia nzima na kila kitu ndani yake. Mara Shetani alipowadanganya, dunia nzima ikaingia dhambini chini ya utawala wa ibilisi, hivyo MUNGU akapanga kuukomboa ulimwengu kwa kushuka duniani kama mwanadamu.[6] MUNGU akawa Mwana wa Mtu. Alijikana NAFSI YAKE kwa ajili yetu, hadi mauti ya NAFSI YAKE pale msalabani, ikifuatiwa na ufufuo na kupaa KWAKE kwenda Mbinguni.[7]

Yohana 3:16 inasema, "Kwa maana jinsi hii MUNGU aliupenda ulimwengu, hata akamtoa MWANAWE wa pekee, ili kila mtu amwaminiye [si Shetani wala mwingine awaye yote] asipotee bali awe na uzima wa milele." Kuwa na maisha ya uzima wa milele inawezekana tu kama KRISTO, ambaye ni MUNGU, Njia, Kweli, na Uzima, anadumu ndani yako kama maisha yako (Yohana 14:6).[8] Huwezi kuwa na uzima wa milele kirahisi kwa kusali sala ya wadhambi. Lazima uwe mwanafunzi pia. BWANA anatuamuru kujitwika msalaba wetu na kumfuata YEYE (Luka 9:23-25).[9] Kuwa na uzima wa milele, hatuwezi kamwe kushuka toka msalabani.[10] Kwa maneno mengine hatuwezi kutenda dhambi tena.

Shetani ni adui aliyeshindwa.[11] Hapo mwanzo, ilionekana kana kwamba shetani alikuwa na mamlaka duniani milele. Lakini leo, kama tukimtii KRISTO na kumkataa Shetani, serikali yake ya duniamoja, na makanisa yake ya ibada za kishetani yanayoongozwa na shetani, mamlaka itakuwa kwetu katika KRISTO.[12]

Jaribio la pili la mwanadamu kumpindua MUNGU na utawala WAKE Mbinguni lilikuwa katika Babeli. Halikufanikiwa, bila shaka. Mwanzo 11:1-9 inazaa kumbukumbu kwamba "Nchi yote ilikuwa na lugha moja na usemi mmoja. Ikawa watu waliposafiri pande za mashariki waliona nchi ya tambarare katika nchi ya Shinari; wakakaa huko. Wakaambiana, Haya na tufanye matofali tukayachome moto. Walikuwa na matofali badala ya mawe, na lami badala ya chokaa. Wakasema, Haya, na tujijengee mji, na mnara, na kilele chake kifike mbinguni, tujifanyie jina; ili tusipate kutawanyika usoni pa nchi yote. BWANA akashuka ili auone mji na mnara waliokuwa wakiujenga wanadamu.

"BWANA akasema, Tazama, watu hawa ni taifa moja, na lugha yao ni moja; na haya ndiyo wanayoanza kuyafanya, wala sasa hawatazuiliwa neno wanalokusudia kulifanya. Haya, na tushuke huko, tuwachafulie usemi wao ili wasisikilizane maneno wao kwa wao [kama *Democrats* na *Republicans* (vyama vya siasa vya Marekani) wasivyoelewana leo, kwa hiyo hakuna la maana linalokamilishwa]. Basi BWANA akawatawanya kutoka huko waende usoni pa nchi yote; wakaacha kuujenga ule mji. Kwa sababu hiyo jina lake likaitwa Babeli; maana hapo ndipo BWANA alipoichafua lugha ya dunia yote; na kutoka huko BWANA akawatawanya waende usoni pa nchi yote."

Jaribio la Shetani la tatu na la mwisho kujaribu kumpindua MUNGU na ufalme WAKE linatokea katika nyakati hizi za sasa. Baadhi ya watu wanasema uongo kwamba UFO wanaowaona wanatoka kwenye sayari nyingine, lakini huu ni uongo. UFO hawatoki sayari nyingine; wanatoka Mbinguni. Sababu natambua hili ni kwa sababu wakati mimi na Susie tulipokuwa tunakwenda Las Vegas kufunga ndoa, tulikuwa kwenye barabara kuu kati ya Los Angeles na Las Vegas usiku sana. Ilikuwa giza wakati Susie, ambaye alikuwa akiendesha gari, alipochukua mkono wangu wa kushoto na akaniambia, "Tony, hebu tumuombe MUNGU na tumuulize ikiwa kuna UFO, tunataka kuwaona." Ni hakika kwamba viumbe kutoka sayari nyingine wasingeweza kusikia sala zetu kwa MUNGU, wala wasingeweza kujibu sala tulizokuwa tukifanya kwa MUNGU. Ghafla, jeshi la UFO likapaa moja kwa moja kwenye kioo cha mbele cha gari letu. Walisogea karibu mno kiasi ambacho nilidhani watatugonga. MUNGU alijibu sala zetu mara moja. MUNGU alipojibu maombi yetu haraka, imani yangu kwa MUNGU na kujibu KWAKE maombi iliimarika.

Ndege zifananazo na magurudumu zimetajwa mara kadhaa katika Biblia.[13] Ni majeshi ya MUNGU ya kifalme ya malaika yakichunguza uovu wa dunia ya leo kabla MUNGU hajakomesha uovu ulio juu ya nchi KRISTO anaporudi. MUNGU huwatuma Malaika katika kipindi hiki cha wakati wa taabu (nasi tuko taabani). Malaika wanatoa taarifa kwa MUNGU, kisha MUNGU huwatuma malaika waharibuo ili kuangamiza maeneo fulani yaliyo maovu katika nchi.[14] YEYE huangamiza kwa tauni (ambayo ni magonjwa), njaa, mafuriko, matetemeko ya ardhi, vimbunga, na nyingine nyingi.

Sehemu kubwa ya watu duniani wanaamini kwamba wanadamu watamshinda MUNGU akili. Wamesahau siku za nyuma, ambapo MUNGU alihatarisha majaribio yao. Shetani alimwambia Hawa kwamba hamtakufa, bali "mtakuwa kama miungu." Lakini alidanganya. Tunatambua hili kwa sababu Hawa na mumewe wote walikufa. Pia, Nimrodi na idadi kubwa ya watu duniani hawakuweza kukamilisha mnara wao, wala hawakujenga Jiji lao Mbinguni. Haikufanikiwa kutokea.

Tena, idadi kubwa ya watu duniani imetumia mabilioni ya dola, na iko tayari kutumia trilioni za dola zaidi, kuhamisha idadi kubwa ya watu kwenda kwenye sayari nyingine, sayari nyingine ambayo wanadhani ina sifa zote za dunia. Lakini

---

**6** Yn. 1:4-13, 12:46, Rum. 5:6-21, Gal. 4:4-5, Ebr. 2:14-18 **7** Mat. 16:21, 20:17-19, 26:31-57, 28:1-10, 16-20, Mk. 10:32-34, Lk. 9:23, Yn. 10:7-18, Mdo. 1:1-11, Gal. 2:20, Fil. 2:5-11, Ebr. 12:1-3, 1 Yn. 3:16 **8** Eze. 36:27, Yn. 14:15-20, 23, 26, 15:3-7, 17:21-23, 26, Rum. 8:10-11, 12:1-2, 1 Kor. 3:9, 16-17, 2 Kor. 6:16-18, Gal. 2:20, Efe. 2:10-22, 3:16-21, Flp. 2:13, Kol. 1:27-29, 2 Tim. 1:14, 1 Yn. 3:24, 4:4, Ufu. 3:19-21 **9** Mat. 16:24-26, Mk. 10:17-30, Lk. 9:59-62, 14:26-27, 33, Yn. 12:24-26, Rum. 8:1-14, 35-37, 12:1-2, 1 Kor. 9:26-27, 2 Kor. 5:9-21, 6:1-10, Gal. 5:16-17, 24, Flp. 3:7-9, Kol. 3:5-17, 2 Tim. 2:4, Tit. 2:12, Ebr. 11:8-26, 1 Pet. 4:1-2, Ufu. 12:10-11 **10** Mat. 10:22, 24:13, Mdo. 14:22, Rum. 11:22, Kol. 1:22-23, 1 Tim. 4:16, 2 Tim. 2:1-3, 3:13-17, 4:5, Yak. 2:17-26, 5:10-11, 1 Yn. 2:24-25 **11** Isa. 14: 9-20, Eze. 28:11-19, Yn. 12:31, 2 The. 2:3-10, Ebr. 2:14, 1 Yn. 2:13-14, 3:8, 4:4, Ufu. 1:18, 12:3-4, 9-12, 20:1-3, 7-10 **12** 2 Kor. 6:14-18, Ufu. 18:1-5 **13** Zab. 68:17, Eze. 1:1-24, 3:12-13, kifu. 10, 11:14-25, Dan. 7:7-9 **14** Mwa. 19:1-25, 2 Sam. 24:1-17, 2 Fal. 19:35, 2 Nya. 32:19-22, Zab. 78:49, Mat. 13:41-42, Mdo. 12:23, 2 The. 1:7-9, Ufu. kifu. 8, 9:1-5, 13-15, 14:8-11, 15-20, 15:1, kifu. 16, 18:1-2, 21, 19:17-21, 20:1-3, 21:9

hakuna sayari yoyote yenye sifa hizo. Ulimwengu uliodanganyika unasubiri kwa shauku kuu kuona upumbavu huu ukitokea. Wameamini mafundisho ya uongo ya serikali moja ya dunia na kanisa la mapepo, vyote vikiongozwa na Shetani, ambaye Mungu alisema kuwa atadanganya dunia nzima katika siku hizi za mwisho (Ufunuo 12:9). MUNGU alisema kuwa Kanisa moja la dunia la Shetani, ambalo linaendesha serikali moja-ya-dunia ya shetani, litakuwa katika mji wa vilima saba (bila shaka hii ni Roma, Vatican, Umoja wa Mataifa).[15] Kama hutambui kuwa Vatican ni mji, unachohitaji kufanya ni kwenda kwenye shirika la usafiri na kuulizia tiketi kwenda mji wa vilima saba. Watakupa tiketi ya Roma, Italia. Tena, hii ni Roma hasa ambayo kishetani inaendesha Umoja wa Mataifa, ambao ni serikali moja ya dunia. Pia inaitwa "*New World Order*" *(Mpango Mpya wa Dunia)* na "kiti cha shetani" (Ufunuo 2:13). NENO LA MUNGU, kupitia Malaika mwenye mapigo saba na Malaika wengine, punde watakuja kuiharibu dunia (na waovu wote).[16]

Ufunuo 17:1-6, 8 inasema, "Akaja mmoja wa wale malaika saba, wenye vile vitasa saba [Vitasa hivi vimejaa mapigo saba ya mwisho yaliyobebwa na UFO, ambavyo kwa kweli ni IFO, vitu vipaavyo vinavyotambulika. Tunaweza kuvitambua IFO kwa kumjua MUNGU na NENO LAKE. MUNGU ni NENO (Yohana 1:1, Ufunuo 19:13).], akanena nami [Malaika huyu alinena nami, Yohana], akisema, njoo huku; Nitakuonyesha hukumu ya Yule kahaba mkuu [Kanisa Katoliki, Vatican] aketiye juu ya maji mengi [mataifa yote ya dunia]: Ambaye wafalme wa nchi [wakuu wote wa serikali, pamoja na majaji wa Vatican na waendesha mashitaka wa Vatican] wamezini naye [kila dhambi mbaya na mateso na mashitaka ya wasio na hatia (watu wa MUNGU)], nao wakaao katika nchi wamelewa kwa mvinyo wa uasherati wake. [Hii inamaanisha kuwa kile wakiitacho usahihi wa kisiasa (kama ndoa za jinsia-moja, ushoga), wapinga-Uyahudi, wapinga-Ukristo, kiu-ya-damu, mauaji, wizi na kila kitu kiendacho kinyume na MUNGU na NENO LAKE.]

"Akanichukua [Yohana] katika ROHO hata jangwani [Ulimwenguni]: nikaona mwanamke, ameketi juu ya mnyama mwekundu sana [Mwanamke ni Vatican, dini-moja ya dunia, na mnyama mwekundu ni Umoja wa Mataifa, ambalo ni gari la Vatican. Linalombeba sehemu mbalimbali ili aweze (mwanamke) kuharibu kazi na watu wa MUNGU kwa Sheria zake za Kanoni. Mwenye] kujaa majina ya makufuru [kama mtu mwenye pepo akichomwa na neno la Mungu, Vatican na serikali moja ya dunia inasema ni uhalifu kumtaja MUNGU katika shule za umma, vyumba vya mahakama, viwanja vya siasa, makumbusho, na maeneo mengine ya kimkakati duniani. Na kwa sababu viongozi wengi katika Kanisa Katoliki ni mashoga, wameunda kanuni mpya, kwamba kupinga ushoga ni dhambi ya kikatili (uhalifu wa chuki). Kuwa na msimamo huu, ni lazima uwe umechukua Alama ya Mnyama katika paji la uso wako (Ufunuo 14:9-11). Hili ni jambo baya sana kiroho.], mwenye vichwa saba na pembe kumi [Hii inatuambia kuwa serikali-moja ya dunia imeundwa na serikali nyingi, yaani, serikali nyingi zimeungana kuwa moja. Zote zinafikiri kwa namna moja; katika hali ya upofu zote zinapokea chochote asemacho Shetani (Ufunuo 17:12-15). Ibilisi hulifanya kuwa jambo la kizalendo unapopokea kila kitu asemacho, na si la kizalendo kama hupokei kila kitu anachosema].

*(Inaendelea ukurasa wa 4)*

**15** Dan. 2:40, 7:19-25, Ufu. 13:1-8, 14:8, kifu. 17, 18
**16** Ufu. 8:7-12, 9:1-11, 15, 14:14-20, 16:2-4, 8-12, 17-21

## Kenya

Kwa huduma ya Tony Alamo,

Salamu kutoka kwetu kwa jina la Yesu Bwana wetu. Naamini kwamba unaendelea vyema na huduma yako. Tungependa kuishukuru huduma yako kwa kututumia maandiko na maombi. Vimepokelewa kwa shukrani sana kanisani kwetu na jamii. Watu wengi wameamua kubadilisha maisha yao na kumkiri Yesu kama Mwokozi wa maisha yao. Na kwa hakika maandiko ya Alamo yamebeba ujumbe wa kweli kwa sababu wakati tunayasambaza, watu wengi waliongoka. Hivyo basi, hii inamaanisha yana ujumbe wa kiroho kutoka kwa Bwana (ni mafuta).

Hivyo basi, ndugu zangu, tumeamua kueneza ujumbe katika vijiji vyote na makanisa kwa sababu unatambua vyema katika Afrika watu wengi bado wanafuata tamaduni za jadi. Kwa sasa tuko watu wapatao 20 walioitwa na kwamba tuna uwezo wa kuwasiliana na watu na kusambaza vitu hivi kwa hekima. Kwa hiyo, tumefanya huduma vema, na bado tunasubiri kile ulichotutumia.

Kuhusu Mchungaji Alamo, Ninaamini kwamba mchungaji wetu atatoka gerezani. Na tunaomba kama timu na kufunga. Na Bwana hatatuacha na Biblia inasema hilo, kama ilivyo katika Zaburi 34:18-19, "BWANA yu karibu nao waliovunjika moyo, Na waliopondeka roho huwaokoa. Mateso ya mwenye haki ni mengi, Lakini BWANA humponya nayo yote." Vita si vyetu bali ni ya Bwana. Pia soma Wafilipi 4:4-9.

Mungu akubariki.
Wako mtiifu,
Mchungaji Moses Kwemboi
Endebess, Kenya



*Mchungaji Moses Kwemboi na baadhi ya mkutano wakisambaza Fasihi za Alamo zinazomshindia roho Bwana maeneo ya Endebess, Kenya.*


**HUDUMA YA MTANDAO YA ALAMO**
**www.alamoministries.com**

## MAJARIBIO MATATU YASIYOFANIKIWA KUMPINDUA MUNGU

*(Inaendelea kutoka ukurasa wa 3)*

"Na mwanamke yule alikuwa amevikwa nguo ya rangi ya zambarau, na nyekundu [hizi ni rangi za dini ya kishetani Kanisa Katoliki], amepambwa kwa dhahabu na kito cha thamani, na lulu [Fedha zote zilizokusanywa na Mamlaka ya Ndani ya Mapato kinyume cha sheria ni mali ya Vatican. Kwa uhalisia wana matrilioni ya dola za kupoteza.], naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake, kilichojawa na machukizo, na machafu ya uasherati wake: [Vatican, ambayo kwa mara nyingine ni kiti cha Shetani, ni chanzo cha kila dhambi duniani, na kuzimu.] Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, LA SIRI, BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA NCHI [maneno 'yameandikwa katika kipaji cha uso wake' kwa lugha rahisi inamaanisha akili yake imefyonzwa katika maovu yote ya kishetani].

"Nikamwona yule mwanamke amelewa kwa damu ya watakatifu [Vatican ya Shetani inafahamika vema kwa umwagaji wote damu duniani, ikiwa ni pamoja na utoaji mimba, maangamizi makuu (holocaust), mauaji ya kikatili ya Kihispania (Spanish Inquisition), na kila vita vilivyowahi kutokea], na kwa damu ya mashahidi wa YESU [Malaika wa BWANA alimwambia Yohana haya]: Nami nilipomwona [Vatican],…Na hao wakaao juu ya nchi, wasioandikwa majina yao katika kitabu cha uzima tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, watastaajabu wamwonapo yule mnyama, ya kwamba alikuwako, naye hayuko, naye atakuwako." "Mnyama ambaye alikuwako" ilikuwa Rumi kabla ya kuanguka, na leo Shetani ameifufua Rumi kwa roho yake ya kishetani, ambayo imekuwa ikitukuzwa kwa vipindi vya dhiki.

Ninapozungumzia mateso na mashitaka ambayo kanisa langu limepitia kwa kipindi cha miaka hamsini, siyazungumzii ili kulalamika au kutafuta kuonewa huruma, lakini kumwonyesha kila mtu kwa mapana ni jinsi gani ni rahisi kuvumilia maovu yote kutoka Kanisa la kishetani la Katoliki, kwa sababu MUNGU amenipa maono. Bila maono watu huangamia (Mithali 29:18). Tunapaswa kufurahi tunapoteswa kwa ajili ya YESU. Itachukua vitabu tele kukuelezea baadhi ya mateso. MUNGU aliniambia kuwa nahitaji kuwa na nguvu mara milioni 100 za kiroho kuliko mti mkubwa wa mwaloni ulioanguka nje ya kanisa langu yapata dakika 15 baada ya kuuambia mkutano kile BWANA alichoniambia.[17] "Heri ninyi watu watakapowachukia, na kuwatenga, na kuwashutumu, na kulitupa nje jina lenu kama neno ovu, kwa ajili ya Mwana wa Adamu. Furahini siku ile na kuruka-ruka, kwa kuwa, tazama, thawabu yenu ni kubwa mbinguni, maana baba zao waliwatenda manabii vivyo hivyo" (Luka 6:22-23).

Nawaambieni mbele za MUNGU na wakaazi wote wa dunia kwamba vile watu waviitavyo UFO havitoki kwenye sayari nyingine, lakini ni Malaika wa Mbinguni. Natoa ahadi ya roho yangu katika hili. Wanaokuambia vinginevyo ni wafuasi wa Shetani waliodanganyika, sawa na Hawa, watu wa Babeli, na Umoja wa Mataifa, na watakupeleka Jehannamu pamoja nao. Ubinadamu hauwezi na kamwe hautachukua nafasi ya MUNGU. Ubinadamu umeshindwa tangu zamani, na utashindwa daima.

YESU KRISTO ni NENO la MUNGU. Amini katika NENO la MUNGU (katika YESU KRISTO), nawe utaokoka

*(Inaendelea ukurasa wa 8)*

**17** Soma "The Tree," Toleo. 6500, "The Most Powerful Position in the Whole Universe," Toleo la. 19700

## India

Ndugu mpendwa katika Kristo,

Mungu akubariki na mwili mzima wa Kristo ndani ya huduma yako. Ni ajabu kutambua kazi kubwa ambayo Mungu amekuwa akifanya kupitia maandiko yako ya injili.

Kwa neema ya Mungu, kwa msaada wa mkutano wetu, leo tulifanya ziara ya Injili katika kijiji cha ndani cha kabila la Dondapudi. Safari yetu (40 km) ilikuwa majini kwa mashua, wanachama thelathini na sita walishiriki. Mungu amefanya kazi kubwa katika kabila la ndani la Hindu kupitia maandiko yako. Ni matumaini yetu yataokoa roho nyingi zilizopotea katika eneo hilo.

Nataka kukutumia picha zetu uone kazi yetu hapa.

Sala zetu ni kwa ajili ya afya ya ndugu yetu Tony na aachiliwe upesi.

Ndugu yako katika Kristo,
Solman Raju Kola
Andhra Pradesh, India







*Ndugu Solman Raju Kola na timu yake ya uinjilisti wakisambaza fasihi za Alamo katika maeneo ya vijiji vya Andhra Pradesh, India.*

## Ushuhuda wa Scott Durning

Nilipokuwa na umri wa miaka 11 au 12, nilipata uzoefu wa kutisha kutoka ulimwengu mbaya wa kiroho ambayo hayafai kurudiwa. Miaka ya baadaye, nilikuja Los Angeles na kuanza kuchukua LSD, na kupoteza mawasiliano na uhalisia kwa miaka michache. Ilikuwa kama milele. Kwa lugha rahisi niliamini nilikuwa nimekufa, na naishi katikati ya maisha kutoka safari mbalimbali za LSD (aina ya madawa ya kulevya).

Siku moja, kwa rehema za Mungu, nilikuwa nikiangalia runinga nyumbani kwa mtu mmoja. Nilichoka hivyo nikaizima. Nilitazama nje ya dirisha la tatu na nilipata maono toka kwa Mungu. Nilikuwa najiona mwenyewe nilipokuwa na umri wa miaka 11, nikiwa nimesimama mbele ya eneo la bustani ya nyumba kule Cleveland, Ohio (ambako ninatoka). Nilijiangalia mwenyewe katika mwendo kasi (sekunde 10) nikikua hadi kufikia umri wangu wa sasa, na nilikuwa nimesimama mbele ya eneo la bustani ya nyumba iliyofuata jirani yetu. Kabla ya kutafakari kwamba jambo hili lilimaanisha nini, Mungu alisema nami. Mungu alisema, "Mungu aliumba jua; Mungu aliumba mwezi; Mungu aliumba dunia; Mungu aliumba nyota; Mungu aliumba majani; na Mungu aliyafanya majani yakue." Nilipatwa na mshtuko. Nikasema hivi kwa sauti, "Ni jua hili hili; ni dunia hii hii; ni mimi huyo. Nilikuwa mkubwa nikachanganyikiwa."

Hili lilinipeleka kwenye uchunguzi, nikitembea mitaani usiku huku nikiongea na Mungu. Baada ya muda, Mungu alinitia hofu mara mbili kwa namna nisiyoweza kuelezea kwa sababu bado nilikuwa nikitenda dhambi. Siku moja nikiwa nimekata tamaa, nilikwenda katika Kanisa la Kikristo la Tony Alamo Hollywood, California. Sikuwahi kwenda kwenye huduma zao kwa sababu halikuwa kanisa "tawala". Ilikuwa yapata saa 11:30 usiku na Tony Alamo alikuwepo pale. Tony alinikabili na kusema, "Unapaswa kukaa hapa." Basi nikafanya hivyo. Usiku uliofuata katika huduma, Wachungaji Tony na Susan Alamo walikuwa pale. Tony alitoa ushuhuda wake kamili jinsi Mungu alivyoongea naye. Sikuwahi kusikia kabla juu ya damu ya Yesu Kristo kuwa ndio ondoleo pekee la dhambi. Kwa nguvu sana nilihisi uwepo wa Roho Mtakatifu. Watu thelathini waliokolewa usiku ule nami nikiwa mmoja wao. Nilikwenda katika chumba cha maombi na kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Nilijua nilikuwa nyumbani. Ilikuwa ni Mei 11, 1970.

Mwaka mmoja na nusu baadaye, nilimwandikia Mchungaji Tony Alamo barua kwa sababu nilikuwa na matatizo. Yapata 2:00 asubuhi, usiku mmoja wa ndugu aliniambia kuwa Tony Alamo alikuwa kwenye simu na alitaka kuongea nami. Nilikuwa kanisani kwetu Saugus, California. Nilichukua simu na kusema, "Salamu, unaongea na Scott." Hakuna mtu aliyejibu chochote. Nilirudia tena mwenyewe. "Salamu, unaongea na Scott." Ndipo nikasikia sauti ya Tony Alamo – "Mungu aliumba jua; Mungu aliumba mwezi; Mungu aliumba dunia; Mungu aliumba nyota; Mungu aliumba majani; na Mungu aliyafanya majani yakue." nilihisi Roho Mtakatifu kama ukuta mkubwa ulionizunguka. Tony Alamo alikuwa akinitia moyo kwa muda wa takribani dakika 45. Sikuwahi kumwambia mtu yeyote kwamba Mungu aliongea na mimi, kidogo zaidi ya aliyosema Mungu.

Kwa miaka mingi, Roho Mtakatifu ameingia katika Injili yote ya fasihi ambazo Mchungaji Alamo anaandika, na ujumbe wote kwa makanisa. Tony na Susan Alamo kwa namna yake wamejenga "miji" katika maeneo mbalimbali ya Marekani kwa ajili ya watu kuishi kwenye Huduma. Jumbe zake za injili zimekuwa zikitumwa kwa posta kwenye nchi 200 tofauti tofauti, kulingana na mahitaji ya watu. Namshukuru Mungu kwamba mimi nimeokoka na nimepata upendeleo kuwa katika Huduma hii.

## Myanmar

Ndugu Tony Alamo,

Salamu nyingi za upendo kutoka Myanmar katika Bwana wetu aliyefufuka na Mwokozi Yesu Kristo. Naomba sana ili mambo yakuendee vizuri.

Tangu 2002, Rod and Staff imeshiriki katika uanzishwaji wa kanisa, uinjilisti, huduma ya matibabu, misaada, shirika la maendeleo ya jamii, mipango ya huduma ya watoto / kituo cha watoto yatima, uzalishaji na usambazaji maandiko kati ya waumini na wasioamini katika Myanmar. Lengo letu ni kufikia watu wasiofikiwa wa makundi yoyote ya kikabila katika Myanmar, na kuwaongoza wasioamini kwa Kristo kwa kugawa maandiko, vijitabu, na Biblia, kufundisha Biblia kwa njia binafsi, vikundi na mikutano ya huduma, na kutafsiri na uchapishaji wa Maandiko ya Kikristo. Tumejitoa kufanya sehemu hii kwa juhudi kuwafikia watu kwa ajili ya Kristo na kuanzisha makanisa mapya.

Nilihamasika na kubarikiwa na maandiko yako, *Masihi kwa kulingana na Unabii wa Biblia*. Tangu wakati huo, nina moto wa kutaka kutafsiri kwa Kiburmese, Hakha-Chin, na Mizo (lugha za makabila ya Myanmar). Kwa sababu kitabu hiki kina nguvu na ninatumaini ni lazima kitakuwa bomba kubwa la Baraka kwa watu wengi. Katika Myanmar maandiko ya Kikristo ni nadra sana, na watu wanaoeneza Injili wamefanya tafsiri, uchapishaji na usambazaji bila malipo. Maandiko ni mema na yenye faida. Asilimia nne tu ya watu hawa ni waumini, lakini sehemu kubwa wamo gizani. Ni maombi yetu kuleta roho nyingi miguuni pa Yesu kwa kupitia maandiko yako. Naamini kwa dhati kuwa kiu ya nyoyo zao itatoshelezwa. (Hakha-Chin na Mizo ni makabila ya watu wanaoishi kilima cha kanda ya magharibi. Wanazungumza lahaja yao wenyewe, na wengi wa watu hawa hawasomi Kiburmese.) Kama unaweza kutuma maandiko yako zaidi kwa ajili ya maktaba yetu tutafurahi sana.

Tunataka sana kupanua huduma yako katika Myanmar. Tuko tayari kufanya kazi nawe kwa ajili yake na tunakualika kupanua huduma yako katika nchi yetu. Kama una muda tunakualika sana kututembelea Myanmar kwa ajili ya Ufalme wake.

Nasubiri kusikia kutoka kwako.
Mungu akubariki.
Katika huduma yake,
Mchungaji Bawi H. Thang, Mkurugenzi
Rod and Staff Ministries
Yangon, Myanmar

http://beforeitsnews.com/celebrities/2014/07/pope-francis-found-guilty-of-child-trafficking-rape-murder-2465728.html

# Papa Francis Apatikana na Hatia ya Ulanguzi wa Watoto, Ubakaji na Mauaji

Jumapili, Julai 20, 2014; 7:28
na Judy Byington



Washitakiwa Papa Francis Bergoglio, Jenerali Mkuu wa shirika la Kikatoliki la Jesuiti Adolfo Pachon, na Askofu Mkuu wa Canterbury Justin Welby; jana walipatikana na hatia ya kufanya ubakaji, mateso, mauaji na ulanguzi wa watoto. Majaji watano wa International Common Law Court of Justice [Mahakama ya Haki ya Kimataifa ya Sheria za Kawaida] huko Brussels walibaini kwamba uhalifu huo ulitendeka hivi karibuni mnamo mwaka 2010. Tangu mwezi Machi, zaidi ya mashahidi 48 wamejitokeza ili kutoa ushahidi mbele ya mahakama hii ya ICLCJ kuhusu shughuli za washitakiwa wakiwa ni wanachama wa shirika la The Ninth Circle Satanic Child Sacrifice Cult [Kundi la Tisa la Dini ya Kizushi ya Kishetani ya Kutoa Watoto Kafara].

Shirika hili la The Ninth Circle Satanic Cult linasemekana kufanya kafara za watoto katika makanisa makuu ya kidayosisi ya Kikatoliki katika miji ya Montreal, New York, Rome, Scotland, London, Carnarvon Castle kule Wales, kwenye Kasri la Kifaransa ambalo halikuwekwa bayana kule Uholanzi, na katika shule za bweni za Kikatoliki za Kikanada na shule za bweni za Kihindi za Kiangiliakana huko Kamloops, British Columbia na Brantford, Ontario Canada. Shirika hili la The Ninth Circle Satanic Child Sacrifice Cult liliaminika kutumia makundi ya misitu inayomilikiwa na watu binafsi nchini Marekani, Canada, Ufaransa na Uholanzi kwa kile kinachoitwa "Sherehe za Uwindaji Binadamu" kwa ajili ya watu mashuhuri duniani zinazojumuisha familia za kifalme za Ulaya. Vijana wenye umri wa kati ya miaka kumi na kitu hivi walikamatwa na [kundi la kiharamia] la mafia, kisha wakavuliwa nguo zote na kuachwa uchi, wakabakwa, wakawindwa na kuuawa. Mwendesha Mashtaka Mkuu alisema:"Kanisa Katoliki ni shirika kubwa zaidi duniani na linaonekana kushirikiana na [kundi la kiharamia] la mafia, serikali mbalimbali, polisi na mahakama mbalimbali duniani kote."

Wasichana wawili walio katika umri wa kupevuka waliiambia Mahakama ya ICLCJ kwamba Papa Francis aliwabaka wakati akishiriki katika utoaji kafara za watoto. Mashahidi wengine wanane walioshuhudia kwa kuona walithibitisha madai yao ya kushuhudia ubakaji na kafara za watoto. Inasemekana The Ninth Circle Satanic Cult ilifanyika wakati wa msimu wa majira ya kuchipua ya mwaka 2009 na 2010 katika maeneo ya vijijini huko Uholanzi na Ubelgiji.

Pia Papa Francis alibainika kuwa mshiriki katika ibada za kishetani za kutoa watoto kafara wakati akiwa padre na Askofu wa Argentina. Hii ni kwa mujibu wa waraka uliotiwa muhuri [waraka wa siri] uliopatikana kutoka kwenye kumbukumbu za nyaraka za kihistoria za Vatican. Waraka wa kumbukumbu wa pili wenye tarehe 25 Desemba 1967 uitwao Magisterial Privilege [Maslahi ya Wenye Mamlaka] ulisemekena kuonesha kwamba kila Papa mpya alitakiwa kushiriki katika Ninth Circle Satanic Cult ya utoaji kafara wa kidini wa watoto wachanga waliozaliwa, ukijumuisha kunywa damu yao. Nyaraka hizi ziliwasilishwa kwenye Mahakama ya ICLCJ na ofisa maarufu wa Vatican na aliyekuwa mwajiriwa katika mahakama ya kipapa ya Vatican.

Mwezi uliopita, mpelelezi wa kikosi cha Irish Garda Police Force alitoa ushahidi mbele ya majaji watano na wafanyakazi 27 wa mahakama kwamba alama zilizokuwa kwenye mifupa ya takribani watoto 796 iliyopatikana katika tanki moja la maji-taka la masista wa Kanisa Katoliki la Ireland zilionesha kuwa walikuwa wameuawa kwa matambiko ya kidini. Shahidi huyo alishuhudia kwamba, wataalamu wa kuchunguza mauaji walithibitisha kwamba ile namna ya kukatwakatwa kwa vichwa na kwa viungo vya miili ya kwenye kaburi la halaiki kulifanana na alama za kawaida za mauaji ya kimatambiko au utoaji kafara za watoto.

Kipindi kimoja cha Shirika la Utangazaji la Uingereza [BBC documentary] kiliweka hadharani kashfa ya miaka hamsini ya biashara ya ulanguzi wa watoto ufanywao na Kanisa Katoliki huko Uhispania. Zaidi ya watoto wachanga 300,000 waliibwa kutoka kwa wazazi wao hadi kufikia miaka ya 1990. Akina mama waliambiwa kwamba watoto wao walifariki na kuzikwa katika makaburi ya watu wengi. Ilisemekana kuwa Kanisa Katoliki lilijipatia dola bilioni 20 kwa kuwauza watoto hao kwa wazazi wapya.

Shahidi mwingine alishuhudia kwamba, walikuwepo wakati wa mikutano kati ya Papa Francis na majeshi ya Junta wakati wa Vita Chafu [Dirty War] vya Argentina mnamo miaka ya 1970. Kwa mujibu wa shahidi huyo, Papa Francis alisaidia ulanguzi wa watoto 30,000 wa wafungwa wa kisiasa waliokuwa hawajulikani walipo na kuwaingiza katika mtandao wa kimataifa wa unyanyasaji watoto unaoongozwa na ofisi iliyoko Vatican.

Katika kipindi cha News Special cha Shirika la habari la ABC ilidokezwa kwamba Ibilisi alikuwa akiishi Vatican. "Nyaraka kutoka makumbusho ya kumbukumbu za siri za Vatican zilizowasilishwa mahakamani zinaonesha wazi kwamba kwa karne nyingi majesuiti walikuwa wamepanga mpango kuwaua kimatambiko watoto waliozaliwa na kuibwa na kisha kunywa damu yao," Mwendesha Mashitaka Mkuu wa ma-

hakama ya ICLCJ aliwaambia wale majaji watano wa kimataifa na wafanyakazi wa mahakama 27. "Mpango huu ulizaliwa kutokana na dhana potovu ya kujipatia nguvu za kiroho kutoka kwenye damu yenye uhai ya wasio na hatia, na hivyo kujihakikishia uimara wa kisiasa wa Upapa huko Rumi. Vitendo hivi si tu vya mauaji ya halaiki bali pia kwa asili yake ni ya kimfumo na ya kitaasisi. Takribani tangu mnamo mwaka 1773, matendo hayo yanaonekana kufanywa na Kanisa Katoliki la Rumi, majesuiti na kila Papa."

Uchunguzi unaoendelea na wa kudumu uliratibiwa ili kuchunguza na kuwafungulia mashtaka watu wengine waliohusika katika uhalifu uliowekwa wazi kwenye mahakama ya ICLCJ. Tarehe 1 Septemba 2014 uchunguzi ulipangwa kuanza wenye jina la Tume ya Kudumu ya Kuchunguza Ulanguzi wa Watoto na Kafara za Kimatambiko [Permanent Commission into Child Trafficking and Ritual Sacrifice]. Hatua za kisheria zaidi zilitarajiwa kufuata.

Mashahidi 48 wa kuona kwa macho waliwatambua wakosaji wao kuwa ni Mapapa wa Kikatoliki Francis Bergoglio, Yohana Paulo II na Joseph Ratzinger; [Kanisa la Anglikana], Kanisa la Muungano la Canada [United Church of Canada] na maofisa wa Kanisa Katoliki wakiwamo Makardinali na Jenerali Mkuu wa Shirika la Kikatoliki la Jesuiti Adolfo Pachon; Malkia wa Uingereza Elizabeth na Mwana Mfalme [Prince] Phillip, Askofu Mkuu wa Anglikana wa Canterbury Justin Welby na Jaji Mkuu wa Mahakama Kuu Fulford; huko Uholanzi: Makardinali wa Uholanzi na Ubelgiji na watu wa jamii za kifalme wakiwamo Mwana Mfalme Mtarajiwa wa Uholanzi Alfrink Bernhard, Mfalme Hendrick, mume wa Malkia Wilhelmina wa Uholanzi, Malkia Beatrix, baba yake na makamu wake, Mwana Mfalme Johan Friso na mke wake Mabel Wisse Smit, mawaziri wa zamani, mkuu wa jeshi la Uholanzi na naibu wa katibu mkuu wa jimbo la Raad; maofisa wa majeshi na serikali za Canada, Australia, Uingereza na Marekani ikiwa ni pamoja CIA ya Marekani [Central Intelligence Agency – wakala wa serikali ya Marekani wa kukusanya taarifa za kiintelijensia], pamoja na mawaziri maarufu serikalini, mahakimu, wanasiasa na wafanyabiashara wa Marekani, Ubelgiji, Uholanzi, Canada, Australia, Ufaransa, Ireland na Uingereza.

Kibali cha kukamatwa kwa Bergoglio na wengine kilitolewa Julai 19, 2014. Kumbukumbu za mahakama zitabaki kuwa siri kwa sasa kwa mujibu wa taarifa ya jana ya vyombo vya habari vya ITCCS. Mahakama ya kwanza ya ICLCJ ilitoa heshima kwa watoto 50,000 wa asili ya Canada waliopotea. Mahakama ilikamilika Februari 2013 kwa kuwahukumu hatia watu 40 mashuhuri duniani pamoja na Malkia Elizabeth.

Watoto hao 50,000 wa asili ya Canada walipotea hasahasa kutoka katika shule za bweni zilizomilikiwa na Kanisa Katoliki. Zaidi ya makaburi ya halaiki 34 ya watoto wachanga yemegunduliwa katika baadhi ya hizo shule za bweni 80 nchini Canada kote. Tangu mwaka 2008 Malkia Elizabeth na Serikali ya Canada wamezidi kukataa maombi ya ITCCS ya kufukua makaburi hayo. Sababu ya maombi haya kukataliwa haikustaajabisha.

Malkia Elizabeth na Mtoto wa Mfalme [Prince] Phillip walikutwa na hatia ya kupotea kwa watoto kumi wa shule ya bweni ya Kamloops huko British Columbia mnamo Oktoba 10, 1964. Tangu wakati huo wazazi hawajapata kuwaona watoto wao. Ufunguzi wa madai haya mahakamani ulisababisha kujiuzulu kwa Papa Ratzinger. Ushahidi kutoka katika kesi hizo unaweza kupatikana katika maandishi ya Kevin Annett ya "Hidden No Longer".

Mahakama ya kimataifa ya ICLCJ ina maofisa wa amani wa Sheria ya Kawaida [Common Law] zaidi ya 450 katika nchi 13, yenye makundi madogomadogo 51 yafanyayo kazi. Fedha za uratibu zilikuwa zikitolewa kwa makundi ya sheria ya kawaida [common law] yaliyokuwa na nia ya kuomba. Ili kuwasiliana na ITCCS, Mahakama ya ICLCJ iliyoko huko Brussels, na washirika wake, au kujitolea, tuma barua pepe au piga simu: itccscentral@gmail.com, hiddenfromhistory1@gmail.com, 386-323-5774 (USA) au 250-591-4573 (Canada).

Kuhusu Mwandishi

Judy Byington, MSW, LCSW, mstaafu, mwandishi wa "Sura Ishirini na Mbili: Ndani ya Maisha yasiyo ya kifani ya Jenny Hill na Nafsi zake Ishirini na Mbili Zaidi" (www.22faces.com) ni mtaalamu wa tiba mstaafu, Mhutubu, Mwanaharakati na Mwandishi wa habari za uchunguzi ambaye makala zake juu ya matukio ya kimataifa ya kashfa za unyonyaji wa watoto zimekuwa zikinukuliwa na mamia ya blogu na tovuti. Msimamizi wa zamani, Kituo cha Afya ya Akili cha Alberta na Mkurugenzi wa Kituo cha Ushauri Nasaha cha Provo Family ni Mkurugenzi Mkuu Mtendaji wa Kuzuia udhalilishaji wa watoto na Baraza la Wasemaji (www.ChildAbuseRecovery.com). Kama una habari zozote kuhusu masuala ya unyanyasaji wa watoto tafadhali tuma barua pepe kwa Judy info@22faces.com. Umealikwa kuliwekea sahihi ombi letu kwa Congress kwa ajili ya kuchunguzwa kwa CIA kuhusu udhibiti wa akili za watoto kwa kubonyesha hapa: http://www.change.org/petitions/us-congress-survivors-request-investigation-cia-mind-control-of-children

## Malawi

Ndugu Mchungaji Alamo,

Asante kwa kututumia habari kuhusu kile kinachofanywa na Kanisa Katoliki kwa ujumla. Napenda kuchukua fursa hii kukwambia kwamba idadi kubwa ya washirika walioungana nasi wanatoka Kanisa Katoliki baada ya kusoma ujumbe wako. Tafadhali endelea kuuhamasisha ulimwengu kuhusu ukweli.

Innocent Mtambo — Chitipa, Malawi

## Ivory Coast

*(Imetafsiriwa kutoka Kifaransa )*

Salamu sana ndugu Pastor Alamo.

Mimi ni Mchungaji Goma Gba Levi. Katika Ivory Coast tumefunga mlango wa Ufalme wa Mbinguni kwa familia chache kwa kisingizio kuwa waume wenye wake wengi hawataingia katika ufalme wa Mungu.

Baada ya kusoma machapisho yako juu ya mitala, na kulinganisha na Biblia, nahamia upande wako. Sasa nafungua mlango huu kwa mapana zaidi. Mungu wa rehema zote na atusamehe.

Pia, naomba chapisho fulani juu ya somo hili na pia "Watoto wengine wa Maria." Ningependa nakala kumi za kitabu cha *Masihi* kwa ajili ya wahubiri wengine ninaowafundisha.

Wako ndugu,

Mchungaji Lévi — Abidjan, Ivory Coast

## MAJARIBIO MATATU YASIYOFANIKIWA KUMPINDUA MUNGU

*(Inaendelea kutoka ukurasa wa 4)*

(Matendo 16:31). Kumkubali KRISTO, NENO LA MUNGU, sali sala hii:

**BWANA wangu na MUNGU wangu, ihurumie roho yangu, mimi mwenye dhambi[18] ninaamini kwamba YESU KRISTO ni mwana wa MUNGU aliye hai.[19] Ninaamini kwamba alikufa msalabani na kumwaga damu yake ya thamani ili nisamehewe dhambi zangu zote nilizozifanya hapo awali.[20] Ninaamini kwamba Mungu alimfufua YESU kutoka kwa wafu kupitia nguvu za ROHO MTAKATIFU[21] na ya kuwa ameketi upande wa kuume wa MUNGU kwa wakati huu akisikiliza maungamo ya dhambi zangu na maombi yangu haya.[22] Ninafungua mlango wa moyo wangu na kukukaribisha moyoni mwangu, BWANA YESU.[23] Nioshe dhambi zangu kwa damu uliyoimwaga kwa ajili ya nafsi yangu pale msalabani Kalivari,[24] hutanikataa, BWANA YESU, utanisamehe dhambi zangu na kuiokoa roho yangu. Ninalijua hili kwa sababu NENO LAKO, yaani Biblia linasema hivyo.[25] NENO LAKO linasema hutamkataa yeyote na mimi nikiwemo.[26] Hivyo ninajua kwamba umenisikia, na ya kuwa umenijibu; na ninafahamu kwamba nimeokoka.[27] Ninakushukuru BWANA YESU kwa kuokoa roho yangu na nitaonesha shukrani zangu kwa kufanya yale unayoniamuru na kwa kutotenda dhambi tena.[28]**

Baada ya kuokoka YESU alisema ni lazima kubatizwa kwa kuzamishwa kabisa kwenye maji mengi kwa jina la BABA, MWANA na ROHO MTAKATIFU.[29] Kwa makini soma Biblia ya KJV, tafsiri ya Kiswahili ya The Bible League, Waenezaji wa Neno la Mungu tangu 1938 na ufanye inavyosema.[30]

BWANA anakutaka uwaambie wengine kuhusu wokovu wako. Unaweza kusambaza makala ya Injili ya mchungaji Tony Alamo. Tutakutumia makala hizi bila malipo. Tupigie simu ama ututumie barua pepe kwa habari zaidi. Mshirikishe na mtu mwingine ujumbe huu.

Iwapo unataka dunia yote iokolewe, kama YESU anavyoamuru, basi usimwibie MUNGU zaka na sadaka zake. MUNGU alisema, "Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote [na dunia hii yote]. Leteni zaka [zaka ni asilimia 10 ya mapato yako yote] kamili ghalani, ili kiwemo chakula [chakula cha kiroho] katika nyumba yangu [roho zilizookolewa], mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema Bwana wa majeshi. Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema Bwana wa majeshi" (Malaki 3:8-12).

---

**18** Zab. 51:5, Rum. 3:10-12, 23 **19** Mat. 26:63-64, 27:54, Lk. 1:30-33, Yoh. 9:35-37, Rum. 1:3-4 **20** Mdo. 4:12, 20:28, Rum. 3:25, 1 Yoh. 1:7, Ufu. 5:9 **21** Zab. 16:9-10, Mat. 28:5-7, Mk. 16:9, 12, 14, Yoh. 2:19, 21, 10:17-18, 11:25, Mdo. 2:24, 3:15, Rum. 8:11, 1 Kor. 15:3-7 **22** Lk. 22:69, Mdo. 2:25-36, Ebr. 10:12-13 **23** 1 Kor. 3:16, Ufu. 3:20 **24** Efe. 2:13-22, Ebr. 9:22, 13:12, 20-21, 1 Yoh. 1:7, Ufu. 1:5, 7:14 **25** Mat. 26:28, Mdo. 2:21, 4:12, Efe. 1:7, Kol. 1:14 **26** Mat. 21:22, Yoh. 6:35, 37-40, Rum. 10:13 **27** Ebr. 11:6 **28** Yoh. 5:14, 8:11, Rum. 6:4, 1 Kor. 15:10, Ufu. 7:14, 22:14 **29** Mat. 28:18-20, Yoh. 3:5, Mdo. 2:38, 19:3-5 **30** Kumb. 4:29, 13:4, 26:16, Yos. 1:8, 22:5, 2 Tim. 2:15, 3:14-17, Yak. 1:22-25, Ufu. 3:18

*Tafadhali wasiliana nasi kwa habari zaidi au kwa vitabu vyetu vyenye mada nyingine ambazo unaweza kuvutiwa nazo:*

**Tony Alamo, World Pastor, Tony Alamo Christian Ministries Worldwide • P.O. Box 2948, Hollywood, CA 90078**

**Namba yetu ya simu kwa ajili ya maombi na habari iliyo wazi kwa saa ishirini na nne ni: (661) 252-5686 • Faksi: (661) 252-4362**

**www.alamoministries.com • info@alamoministries.com**

*Huduma ya Tony Alamo Christian Ministries Worldwide hutoa mahali pa kuishi pamoja na vitu vyote muhimu kwa maisha kwa wale walio Marekani ambao wanataka kumtumikia BWANA kwa mioyo yao yote, roho zao zote na nguvu zao zote.*

**Huduma yetu hufanyika jijini New York kila Jumanne, saa mbili usiku na mahali pengine kila usiku.**

**Tafadhali wasiliana nasi kupitia simu namba (908) 937-5723 kwa habari zaidi. CHAKULA HUTOLEWA BAADA YA KILA IBADA.**

**Tuma maombi ujipatie kitabu cha Mchungaji Alamo kiitwacho, The Messiah, kinachomwonesha KRISTO alivyo katika Agano la Kale kwa jumbe za unabii zipatazo 333.**

*Kuwa mmoja wa watumishi katika kuvuna roho za watu kwa kuwa msambazaji wa makala na vitabu vya Mchungaji Alamo*

*Machapisho yetu na jumbe kwenye tepu za sauti hayalipishwi kitu ikiwemo gharama ya kusafirisha kupitia meli.*

*Iwapo kuna mtu atajaribu kukulipisha, tafadhali tupigie simu kwa namba: (661) 252-5686.*

**MAKALA HIZI ZIMEBEBA MPANGO WA KWELI WA UKOMBOZI (Matendo ya Mitume 4:12)**
**USIZITUPE: ZIFIKISHE KWA MTU MWINGINE.**

**Kwa wale ambao mko kwenye nchi nyingine, tunawashauri kutafsiri makala hizi kwa lugha zenu. Iwapo mtachapisha tena, tafadhali jumuisha haki hii na usajili:**

© Hatimiliki Agosti 2014, 2015 Haki zote zimehifadhiwa Mchungaji wa Dunia Tony Alamo ® Imesajiliwa Agosti 2014, 2015

SWAHILI—VOLUME 20100—*THREE UNSUCCESSFUL ATTEMPTS TO OVERTHROW GOD*